*Mulika, Na. 44 (1), 36-59*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uchanganuzi wa Fani katika Kuakisi Dhamira za Kiteolojia katika Diwani Teule za Kiswahili

*Eric Ndumbaro*[1], *Leonard Ilomo*[2] *na Joviet Bulaya*[3]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t1.3

**Ikisiri**

Makala haya yanachunguza jinsi vipengele vya kifani vinavyotumika kuwasilisha dhamira za kiteolojia katika ushairi andishi wa Kiswahili. Ingawa baadhi ya wanazuoni, mathalani, Trilling (2008), wanapinga kuwapo kwa uhusiano kati ya fasihi na teolojia, wakisisitiza kuwa fasihi haipaswi kuhusishwa na masuala ya kiteolojia, kuna hoja zinazopinga msimamo huo. Crosby (2022) anaeleza kuwa mitazamo ya kihistoria kuhusu teolojia na fasihi, hasa mwishoni mwa Zama za Kati, ilifanya baadhi ya watu, kutilia shaka ufanisi wa fasihi katika kueleza ukweli wa kiteolojia. Kutokana na mitazamo hiyo, kazi za waandishi kama vile Donne, Herbert, na Vaughan hazikutambuliwa kutokana na kuhusisha kazi zao na masuala ya teolojia (Calloway, 2023). Hata hivyo, Watson (2022) anakosoa mitazamo hiyo kwa kusema kuwa kuna kuchanganya kati ya teolojia na dini. Anaeleza kuwa teolojia ni taaluma inayojadili uhusiano kati ya nguvu kuu (kama Mungu) na viumbe, ilhali dini ni mfumo wa ibada na kujisalimisha kwa nguvu hizo. Teolojia, kwa hivyo, ni taaluma ya kiakademia inayochunguza imani, maadili, na maisha ya umilele. Katika kuchunguza dhihiriko la dhamira hizo, makala haya yamejikita katika diwani mbili: *Wino wa Kalamu Ndogo* (2019) na *Ngonjera Zetu 1* (2020). Ili kufikia lengo hilo, makala yametumia mbinu ya usomaji makini na Nadharia ya Udhanaishi. Matokeo yanaonesha kuwa vipengele vya kifani kama taswira, muktadha, mtindo, na matumizi ya lugha vinatumika kuakisi dhamira za kiteolojia. Inapendekezwa tafiti zaidi zifanyike kwa lengo la kulinganisha dhamira za kidini na kiteolojia ili kuelewa tofauti kati ya dhana hizo katika fasihi ya Kiswahili.

## 1.0 Utangulizi

Upo mkanganyiko mkubwa unaojitokeza katika tafiti na chambuzi anuwai za kitaaluma kuhusu dhahira[4] ya kazi za fasihi andishi ya Kiswahili hususani dhamira.

[1] Mwanafunzi wa Uzamivu, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: erindumbaro@yahoo.com.

[2] Mhadhiri, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: ilomo.leonard@udsm.ac.tz

[3] Mhadhiri, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: jovietbulaya@yahoo.com.

Baadhi ya dhamira zinazojadiliwa katika tafiti na chambuzi hizo zimeegemezwa zaidi katika mtazamo wa kidini (Njoroge, 2001; Lodhi, 2010; Malugu, 2016; Watson, 2022) ilhali hazina uhusiano wa moja kwa moja na masuala ya dini. Changamoto inayoonekana kutokana na mkanganyiko huu ni kushindwa kwa watafiti na wachambuzi kutofautisha dhahiri dhamira za kiteolojia na dhamira za kidini katika fasihi andishi ya Kiswahili. Mathalani, watafiti na wachambuzi wa fasihi andishi ya Kiswahili mara nyingi hutumia dhana hizi mbili kwa pamoja bila kudadavua kinagaubaga utofauti uliopo. Hali kama hii inasababisha kutoeleweka kwa dhamira husika na kuongeza ugumu katika kuelewa muktadha unaoibua dhamira hizo kama ni wa kiteolojia, kidini, au kifalsafa kulingana na kazi husika.

### 1.1 Dhana ya Dhamira

Dhamira ni dhana mojawapo inayohusika katika kujenga maudhui ya kazi za fasihi. Dhana hii hurejelea masuala anuwai yanayojadiliwa na kazi mbalimbali za fasihi (Senkoro, 2011). Wazo hili linaungwa mkono na Carter na Carter (2014) wanapobainisha aina kumi za dhamira au mawazo makuu yanayotawala katika fasihi ambayo ni matumaini, kukata tamaa, mafanikio, uvivu, usaliti, kisasi, shauku, udadisi, mashaka na upendo. Wataalamu Carter na Carter (2014) wanadai kuwa, dhamira zote kumi hazijitokezi sana katika uchambuzi wa kisosholojia. Dhamira zilizobainishwa tunaweza kuzitenga katika makundi makuu manne: dhamira za kisiasa, dhamira za kijamii, dhamira za kitamaduni, na dhamira za kiteolojia na kifilosofia. Dhamira, katika makundi yote manne, hudhihirisha lengo au wazo la jumla lililofumbata na linaloibuliwa na msomaji wa kazi husika ya fasihi. Aidha, lengo kuu la utengaji wa dhamira hizi ni kuwasaidia wachambuzi kupata urahisi wa kulinganisha na kulinganua dhamira zinazolandana au zinazosigana, jambo ambalo litarahisisha ufafanuzi na kuongeza uelewekaji wa mada. Katika muktadha wa makala haya, dhamira zitakazojadiliwa ni dhamira za kundi la nne hususani zile zinazohusu masuala ya kiteolojia tu.

### 1.2 Dhana ya Teolojia na Dini

Teolojia ni uwanja wa falsafa inayojikita katika tafakuri ya uhusiano wa Nguvu Asili na viumbe wengine hususani binadamu kupitia matawi yake anuwai kama vile anthropolojia na eskatolojia neumatolojia, maadili na soteriolojia (Croitoru, 2020; Pamplany na wenzake, 2021). Katika fasihi ya Kiswahili, dhana hizi za kiteolojia hazijibainishi katika dhamira zinazohusu maisha ya binadamu kama sehemu ya imani tu, bali kama mjadala wa kiteolojia na kifasihi unaoangazia maswali muhimu kuhusu

---

[4] Katika muktadha wa kifasihi, istilahi ‘dhahira’ inarejelea vipengele vinavyojitokeza wazi na kuvuta umakini wa msomaji wa matini za kifasihi.

uhusiano wa Nguvu Asili na binadamu, hatima ya binadamu, uumbaji, kifo, hukumu, wokovu na maisha baada ya kifo. Waandishi wa fasihi ya Kiswahili kama vile Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi wametumia dhana hizi kutunga mashairi yanayochunguza masuala ya kiroho, mateso na dhambi kwa mtindo wa kifalsafa. Aidha, badala ya kutumia teolojia, wao wamekuwa wakitumia dini kama zana ya kuelezea uhusiano uliopo baina ya binadamu na Mungu. Pia, mtazamo huu wa kuinasibisha dhana ya teolojia na dini unasadifu mawazo ya Kinara na wenzake (2024) wanaoeleza kwamba heshima, adabu, utu wema na bidii havitazamwi kama dhana za kiteolojia bali kama dhana za kidini zinazojenga utangamano wa wanajamii na Mungu kwa jumla.

Kwa minajili hiyo, dini huchukuliwa kama mfumo wa imani na ibada zinazohusisha utekelezaji wa maadili ya kiroho na kijamii katika jamii (Berry, 2023). Dini, tofauti na teolojia, inaelezea na kuongoza matendo ya kijamii na kitamaduni kama vile ibada, sala na maagizo ya kimaadili (Durkheim, 2001; Watson, 2022). Hivyo, dini inahusisha utekelezaji wa imani katika maisha ya kila siku, ilhali teolojia inamakinikia mjadala wa kiakili na kifalsafa kuhusu uhusiano wa mwanadamu na Nguvu Asili, uumbaji, maadili, mateso, kifo, hukumu, na wokovu. Mathalani, katika fasihi andishi ya Kiswahili, tunaona Jesse na King'ei (2019) wanatuonesha namna mwandishi Said Ahmed Mohamed katika *Dunia Yao* na *Mhanga Nafsi Yangu* anavyotumia mifumo ya kidini na kiimani kuonesha mapambano ya kijamii na kiroho, lakini wanashindwa kutofautisha masuala ya kiteolojia na masuala ya kidini kama vile ibada, peponi na motoni, jambo ambalo linachanganya muktadha wa dhana hizi mbili.

Katika tafiti za wataalamu tuliowapitia kuhusu dhana ya teolojia katika fasihi andishi, haijawekwa bayana tofauti kati ya masuala ya kiteolojia na ya kidini. Hivyo, makala haya yanachambua dhamira za kiteolojia zilizobebwa na vipengele vya fani katika diwani teule.

## 2.0 Nadharia Zilizotuongoza

Uchanganuzi wa vipengele vya kifani vinavyoakisi dhamira za kiteolojia uliongozwa na Nadharia ya Umtindo na Nadharia ya Udhanaishi. Nadharia ya Umtindo imetumika kubaini mbinu za lugha na namna dhamira zinavyowasilishwa kifani, wakati Nadharia ya Udhanaishi imetumika katika kuchambua maudhui na jinsi yanavyoelezwa. Uteuzi wa nadharia hizi ulifanywa kwa kuwa zote zinajengana kimantiki na zina uwezo wa kuchambua vipengele vya lugha na kuibua dhamira mbalimbali za kiteolojia katika ushairi wa Kiswahili.

## 2.1 Nadharia ya Umtindo

Nadharia hii iliongoza uchanganuzi wa vipengele vya kifani vinavyoakisi dhamira za kiteolojia. Kama taaluma, Umtindo ulianza kujitokeza mwishoni mwa karne ya 19 na mwanzoni mwa karne ya 20 kwa lengo la kuelezea mitindo ya waandishi katika kazi zao. Mwanzo wa Umtindo unahusishwa na kuibuka kwa isimu sinkroniki au isimu mamboleo, hasa kupitia mawazo ya Ferdinand de Saussure (1857–1913), mwasisi wa isimu mamboleo. Mawazo haya yaliwekwa msingi na mwanafunzi wake, Charles Bally (1865–1947), ambaye alianzisha nadharia ya Umtindo. Kwa mujibu wa Ammon (1989), Bally alithibitisha mwaka 1909 kwamba, Umtindo ni taaluma tofauti na isimu ya Saussure, kwani ulizaliwa ndani ya isimu lakini baadaye ukapanuka hadi kwenye fasihi na taaluma nyingine.

Nadharia ya Umtindo ni mawazo ya kitaaluma yanayozingatia uwasilishaji wa vipengele vya lugha katika matini za kiisimu na kifasihi (Leech na Short, 1981), ikiwa kama daraja kati ya taaluma ya isimu na fasihi. Kwa msingi huo, nadharia hii huunganisha nyanja anuwai za kisarufi zinazohusiana na vipengele vya ndani na vya nje vya kazi ya kifasihi (Barry, 2002). Katika uhakiki wa matini za kifasihi, Umtindo hushughulikia vipengele vya lugha vinavyojenga maana msingi na maana fiche, pamoja na mbinu kama tamathali za semi, mandhari, taswira, vielelezo, ishara na kile kinachoashiriwa (Leech, 2008). Kwa kuwa fasihi hutumia lugha, haiwezi kuepuka viwango vya umtindo vinavyohusiana na isimu, kama vile grafolojia, fonolojia, leksikolojia, sintaksia, semantiki, na pragmatiki.

Kwa ujumla, Umtindo katika uchambuzi wa vipengele vya fani katika matini za kifasihi huhusiana na mwandishi, maandiko, msomaji na mandhari. Magair (2013) anasisitiza kuwa matokeo ya utendaji wa lugha ndiyo yanaunda ujumi ambao lugha na fasihi hutumia kuwasilisha wazo katika kazi ya sanaa. Naye Tariq (2018) anabainisha elementi sita muhimu za umtindo anazoziita "rubriki[5]" ambazo ni: mtindo kama ukiushi wa kaida au kawaida, upekee wa mtu binafsi, maudhui na/au umbo la maandishi, uchaguzi kati ya njia mbadala za kuelezea wazo lilelile, matokeo ya muktadha na uandishi mzuri au unaovutia.

Elementi hizo zina uhusiano mkubwa na misingi ya Nadharia ya Umtindo kama ilivyoelezwa na Leech (1969, 2008). Leech anaweka misingi sita ya nadharia hii ambayo ni: mosi, ni vigumu kubainisha maudhui na fani bila kurejelea elementi za kiisimu; pili, lugha humruhusu mwandishi kufanya uchaguzi mbalimbali wa kuwasilisha mawazo yake; tatu, uchaguzi wa kipengele cha lugha hufanywa kulingana

[5] Seti ya maagizo au kanuni

na dhamira au muktadha; nne, hisia hudhihirishwa kupitia matumizi ya vipengele vya lugha; tano, umtindo husaidia kuelewa matumizi ya msamiati na kuchambua kilongo pamoja na fasihi; na sita, mbinu ya urudiaji husaidia kuibua dhamira na ujumbe. Misingi hii imetumika kuchunguza vipengele vya kifani vinavyoakisi dhamira za kiteolojia katika diwani teule.

## 2.2 Nadharia ya Udhanaishi

Uchanganuzi wa dhamira za kiteolojia katika diwani teule uliongozwa na Nadharia ya Udhanaishi, ambayo huzingatia uchunguzi wa uwepo, uhuru, na harakati za maisha ya mwanadamu pamoja na uhusiano wake na nguvu zinazomzidi (Mungu). Udhanaishi ni mawazo ya kifalsafa na kiteolojia yanayochambua maisha ya mwanadamu, nafasi na jukumu lake duniani, pamoja na athari za uhusiano wake na nguvu zilizo juu ya uwezo wake (Sartre, 1970; Kierkegaard, 1974; Wyschogrod, 1982). Kwa mujibu wa wanaudhanaishi kama Martin Heidegger (1889–1976), Gabriel Marcel (1889–1973), na Albert Camus (1913–1960), mwanadamu ni kiumbe huru anayejitahidi kutafuta maana katika ulimwengu usio na maana dhahiri, huku akiwa na jukumu la kuwajibikia matokeo ya matendo yake na uchaguzi wa maisha yake (Camus, 1984).

Tangu awali, Jean-Paul Sartre, mwasisi wa Nadharia ya Udhanaishi, alijikita katika kujibu swali: "Ni nini maana ya maisha?" Tofauti na wanafalsafa wengine, Sartre (2007, 2008) anasisitiza kuwa, kwa asili, maisha hayana maana—yanafanywa kuwa na maana kupitia jinsi tunavyoishi na uchaguzi tunaofanya. Kwa mujibu wake, "maisha yenyewe si chochote mpaka tunapoyaishi; ni sisi tunaoyapa maana […]" (Tafsiri yetu). Hii inaonyesha kuwa thamani ya maisha inategemea uhuru wa binadamu kuamua matokeo, kuchagua njia, kuwajibika, na kutenda, kwani sisi ni kile tunachojiumba kupitia vitendo vyetu.

Aidha, kwa mtazamo wa wanaudhanaishi wanaoamini uwepo wa Mungu, Mungu ndiye chanzo cha maana ya maisha, hivyo harakati zote za kutafuta maana hupaswa kuelekezwa kwake; la sivyo, maisha huwa ubatili. Anayeamini uwepo wa nguvu hizo hutenda yanayompendeza Mungu, yaani maadili ya Kimungu. Pia, mwanadamu anapokabiliana na changamoto zinazozidi uwezo wake kama vile maumivu, mateso, kifo, maradhi na majanga hujisalimisha kwa Mungu ili kupata faraja au suluhisho. Kitendo hiki huimarisha uhusiano wake na nguvu hizo zilizomuumba na kumpa nafasi ya kuishi duniani.

Nadharia ya Udhanaishi imekuwa na mchango mkubwa katika fasihi, hasa ushairi wa karne ya 20 na 21 (Falconer, 2019; Bora, 2020). Washairi kama vile Mathias Mnyampala (*Diwani ya Mnyampala*, 1965), Shaaban Robert (*Insha na Mashairi,*

1967), Euphrase Kezilahabi (*Kichomi*, 1974; *Dhifa*, 2008), Kithaka wa Mberia (*Mchezo wa Karata*, 2010; *Rangi ya Anga*, 2014) na Rehema Mbwambo (*Kimya*, 2020) wameangazia mada za kifalsafa na kiteolojia kupitia mtazamo wa udhanaishi, kama vile upuuzi wa maisha, utafutaji wa maana, uhuru, kifo, uhai, Mungu, maadili, haki, na asili ya mwanadamu. Nadharia hii hujitokeza katika ushairi kwa njia ya tafakuri kuhusu maisha, hofu, huzuni, hali ya binadamu, na mapambano ya kila siku.

Nadharia ya Udhanaishi ni faafu katika kuchambua maisha ya mwanadamu kwa mtazamo wa kiteolojia kwani inazingatia hali ya mtu binafsi, uhuru wa maamuzi, na mapambano ya ndani kuhusu maisha, kifo, na uhusiano na Mungu. Inasisitiza kwamba imani na maamuzi ya kiroho yanapaswa kuwa ya hiari, si ya kulazimishwa na jamii au dini. Suala hili ni muhimu katika teolojia kwa kuwa udhanaishi hulenga dhamira ya mtu binafsi na uwajibikaji wake kwa Mungu. Dhamira kama vile imani, toba, msamaha na wokovu huangaliwa kwa mtazamo wa ndani. Wanafalsafa kama Kierkegaard na Sartre walieleza misingi ya udhanaishi, ikiwa ni pamoja na utegemezi wa mwanadamu kwa Mungu, imani kama msingi wa maana ya maisha, maadili ya kimungu, uhuru na uwajibikaji binafsi, maisha kama safari ya kuelekea kifo, na changamoto za maisha zinazotikisa utulivu wa kiroho na kifikra.

Hivyo, ingawa misingi ya udhanaishi imetuongoza kuchambua dhamira za kiteolojia katika diwani teule, msomaji au mhakiki anapaswa kuelewa kuwa udhanaishi humchukulia msomaji au mhakiki kama mtu binafsi anayesoma matini kwa misingi ya uhuru wake wa kiutambuzi, hisia, uzoefu, imani, hofu, na mapambano ya kiroho au kiakili. Mtazamo huu humsaidia msomaji kuelewa vyema dhamira na malengo ya matini anayochunguza.

## 3.0 Methodolojia

Data katika makala haya ilikusanywa kupitia usomaji makini wa matini na uchambuzi wa nyaraka kutoka katika diwani *Wino wa Kalamu Ndogo* (2019) na *Ngonjera Zetu 1* (2020). Vipengele vya kifani vilivyotumiwa na waandishi kuwasilisha dhamira za kiteolojia vilibainishwa, pamoja na dhamira hizo kulingana na matawi ya teolojia kama anthropolojia, neumatolojia, maadili, na soteriolojia. Uchambuzi ulifanywa kwa mashairi kumi na moja, matano kutoka *Wino wa Kalamu Ndogo* na sita kutoka *Ngonjera Zetu* 1, kwa kutumia misingi ya Nadharia ya Umtindo na Nadharia ya Udhanaishi.

## 4.0 Vipengele vya Kifani na Dhamira za Kiteolojia

Kipengele hiki kinawasilisha uchanganuzi wa vipengele vya kifani ambavyo vimebainika kubeba dhamira za kiteolojia katika diwani za *Wino wa Kalamu Ndogo* (2019) na *Ngonjera Zetu 1* (2020).

### 4.1 Taswira

Kipengele cha taswira kimeibuka kutokana na idhini ya kishairi aliyonayo mtunzi katika kutumia lugha vile apendavyo kwa malengo maalumu. Katika shairi la 'Rangiye Kaniki' mtunzi anatumia mbinu ya udondoshaji wa sauti /a/ katika silabi 'ya' na sauti /k/ katika silabi 'ke' na kisha kuunganisha sauti hizo na neno rangi-*ye* ili kujenga dhana ya urejeshi. Pia, anafupisha maneno kwa kudondosha silabi 'ya' ili kutofautisha lugha ya kinudhumu (rangiye kaniki) na lugha ya kinathari (rangi yake ya kaniki). Uhuru huu wa mtunzi unaelezwa katika msingi wa tano wa Nadharia ya Umtindo kwamba mtunzi ana uhuru wa uchaguzi wa msamiati unaotumika kuwasilisha na kupokea maana ya ujumbe, pamoja na kuchambua diskosi na fasihi. Mathalani, katika ushairi mtunzi anaruhusiwa kutumia anafora au epifora au kudondosha sauti au neno kwa malengo mahususi.

Taswira, kama inavyoelezwa kupitia Nadharia ya Umtindo, ni dhana iliyochambuliwa kwa kina na watafiti wa fasihi kama vile Wamitila (2003, 2004) na Kress na Van Leeuwen (2020). Kimsingi, wote wanakubaliana kuwa taswira ni picha ya kisanaa inayoweza kuwa wazo, hali, dhana, mwonekano wa kitu au uzoefu wa kijamii unaojengeka akilini au machoni mwa mtu, na ambayo huficha maana ya ndani isiyo dhahiri. Kress na Van Leeuwen (2020) wanaongeza kuwa taswira hujenga maana kwa njia tatu: mosi, kupitia uwakilishi wa moja hali au jambo fulani; pili, kupitia mwingiliano baina ya fikra za msomaji, mtazamaji au msikilizaji, yaani namna inavyoathiri hisia na mtazamo wake; na tatu, kwa njia ya muundo, ambapo vipengele kama tamathali za semi hupangwa pamoja ili kuunda taswira yenye maana.

Hivyo, katika uchambuzi wa data tumebaini kuwa, taswira zilizotumiwa na mtunzi wa diwani ya *Wino wa Kalamu Ndogo* zimeakisi dhamira anuwai za kiteolojia. Kwa kurejelea, shairi la 'Rangiye Kaniki' linaibua maswali makuu kuhusu nafasi ya Mwafrika katika kudumisha utamaduni. Kwa kutumia teolojia tunaweza kuchunguza jinsi anthropolojia kama tawi la teolojia linavyoathiri tafakuri za hisia na fikra za jamii kuhusu utamaduni. Ushairi wa Kiswahili una uwezo wakusawiri masuala ya utamaduni na athari zake kwa jamii kupitia vipengele vyake vya kifani. Mathalani, kwa kutumia ufundi mkubwa wa lugha, (udondoshaji wa sauti na uteuzi wa msamiati) mwandishi anajenga taswira inayoibua dhamira ya utamaduni kama inavyodhihirika katika beti zifuatazo:

1. Ni **nyeusi** fii, rangiye **kaniki**
**Na haififii**, **hata kwayo jiki**
Mfanye bidii, haibadiliki
Rangiye kaniki.

2. Wakina nanii, mapapa samaki
Hawaisifii, hata kinafiki
**Haipo zii**, na **haichujiki**
Rangiye kaniki.

(uk. 16)

Mwandishi anateua maneno kama 'nyeusi' na 'kaniki' kujenga mwonekano wa mtu mweusi, yaani Mwafrika. Pia, anataja kiumbe cha majini 'mapapa samaki' kujenga taswira ya mataifa makubwa ya Kimagharibi ambayo hayaoni thamani ya utamaduni wa mtu mweusi. Aidha, msingi wa tatu wa Nadharia ya Udhanaishi unadai kuwa mwanadamu husukumwa kutekeleza matakwa ya nguvu zilizomuumba katika kutii kanuni za kimaadili zilizowekwa na nguvu hizo. Kwa minajili ya msingi huu, ni wazi kwamba baadhi ya masuala ya kimaadili katika kijamii husika kama vile kuthamini utamaduni hutekelezwa pasi shuruti kutokana na msukumo wa ndani alionao mtu. Kwa ujumla, kipengele hiki cha taswira kinaakisi dhana ya utamaduni kama dhamira muhimu ya kiteolojia kupitia tawi la anthropolojia ya utamaduni. Katika anthropolojia ya utamaduni, lugha hutazamwa kama chombo cha kuendeleza tafakuri za kiroho na kijamii. Hivyo, licha ya msukumo uliomo ndani ya kila mwanadamu katika kutii kanuni na matakwa ya jamii yake, mwandishi anaiasa jamii ya Kiafrika kutafakari kwa kina asili, uzuri na thamani ya rangi ya Mwafrika na kisha kuionea fahari. Hakuna taifa la ng'ambo litakalomsaidia mtu mweusi kulinda na kuthamini utamaduni wake zaidi ya yeye mwenyewe.

## 4.2 Mtindo – Usimulizi wa Kimonolojia na Kidayalojia

Dhana ya mtindo imejitokeza kupitia matumizi ya nafsi ili kuonesha namna mbinu (monolojia na dayalojia) za usimulizi zinavyoweza kuibua athari fulani katika matini. Kwa kurejelea msingi wa nne wa Nadharia ya Umtindo unaodai kuwa udhihirisho wa hisia katika lugha unahusiana moja kwa moja na kazi ya elementi za lugha. Vipengele hivi viwili huingiliana na kushirikiana ili kusaidia kuwasilisha mawazo. Msingi huu unaonesha namna elementi za lugha (vitamkwa au viambishi vya nafsi) vinavyohusiana na dhana ya hisia katika kudhihirisha upekee wa mtunzi kupitia mtindo wa kuwasilisha wa hisia kama itakavyodhihirika baada ya kujadili dhana ya mtindo.

Mtindo ni upekee wa mwandishi katika uundaji wa kazi yake ya fasihi unaomtofautisha na mwandishi mwingine (Wamitila, 2004). Unajumuisha mbinu

mbalimbali za kisanaa zinazolenga kuvutia hadhira na kutimiza lengo la mwandishi. Vipengele vya mtindo ni pamoja na uteuzi wa maneno, mpangilio wa viambishi au vitamkwa, matumizi ya lugha mseto, lugha ya nathari, tamathali za semi, na mbinu za kiusimulizi kama taswira, fomula simulizi, takriri, monolojia na dayalojia (Mulokozi, 2017). Baadhi ya mbinu hizi zimetumiwa na waandishi wa diwani teule, kama inavyoonekana katika Wino wa Kalamu Ndogo kupitia mashairi ya *'Waja Tuyatende Mema'* na *'Anenayo Mwanadamu'*.

### 4.2.1 Usimulizi wa Kimonolojia

Msingi wa kwanza wa Nadharia ya Umtindo unaeleza kuwa si rahisi sana kubainisha na kufafanua vipengele vya kifani katika matini za kifasihi pasi kurejelea elementi anuwai za kiisimu. Tukirejelea viambishi vya nafsi kama elementi ya kiisimu tunaona kwamba mwandishi ametumia monolojia kama mtindo wa usimulizi unaohushisha matumizi ya nafsi zote tatu kama inavyoonekana katika shairi lifuatalo la 'Waja Tuyatende Mema':

3. **Ndivyo hivi *na*ja ndani**, ***ni***ufikishe ujumbe
Ndilo neno la thamani, **sikio lenu niombe**
Linenwa tangu zamani, wakapuuza wazembe
**Waja tuyatende mema, ili tupate ya heri.**

Yupi aliyetambuwa, **shani ya matendo mema**?
Mikono kuikunjuwa, kwa **wajane** na **yatima**
Tusiwe fundo la muwa, barakaze zikakwama
Waja tuyatende mema, ili tupate ya heri.

**Mwenyezi** hataki pesa, ndipo **atuneemeshe**
Moyo upigwe msasa, mbegu bora tuoteshe
Haya alishatuasa, rejea tujikumbushe
Waja tuyatende mema, ili tupate ya heri.
(uk. 22)

Mtindo huu umezoeleka zaidi katika matini za kinathari zenye mtiririko wa visa na matukio. Kwa hiyo, unapotumika katika nudhumu licha ya kuonesha upekee wa mwandishi, pia husaidia kuakisi dhamira kwa urahisi zaidi pasi na kificho. Mathalani, matumizi ya viambishi vya nafsi kama 'na' katika neno *naja*, 'ni' katika neno *niufikishe* huonesha nafsi ya kwanza umoja ambapo mtunzi anawasilisha hisia zake binafsi. Kadhalika, shairi la 'Waja Tuyatende Mema' linaonesha maudhui yenye uzito wa kiroho na kijamii, likisisitiza nafasi ya mtu binafsi katika kuchagua njia yake ya kiroho dhidi ya dhambi na maovu. Mwandishi anatumia mtindo wa usimulizi kama kipengele cha kifani katika kuakisi dhamira ya matendo mema. Mwandishi anaiasa jamii umuhimu wa kutenda matendo mema kama njia ya kujiwekea hazina siku za usoni. Kimsingi, dhamira ya matendo mema ni ya kiteolojia iliyofumbatwa katika

tawi la maadili. Suala la kutenda mema ni suala la kimaadili linalotokana na Nguvu Asili inayomfanya mwanadamu kuona hitaji hilo. Msingi wa tatu wa Nadharia ya Udhanaishi unathibitisha hilo kwa kueleza kuwa mwanadamu husukumwa kutekeleza matakwa ya nguvu zilizomuumba katika kutii kanuni za kimaadili zilizowekwa na nguvu hizo. Kwa mfano, anatumia neno 'Mwenyezi' akirejelea hiyo Nguvu Asili ambayo pia hutoa neema kama tuzo au mshahara wa matendo mema. Baadhi ya matendo mema ambayo mwandishi anabainisha ni pamoja na kuwasaidia yatima na wajane, kundi ambalo anaona kama limetelekezwa na jamii ya leo.

Kadhalika, kipengele cha mtindo kinajitokeza tena katika shairi la 'Anenayo Mwanadamu'. Mtindo wa usimulizi umetumika katika kuakisi dhamira ya maadili ambayo pia ni tawi mojawapo la taaluma ya teolojia. Kupitia kipengele cha mtindo, mwandishi anatumia mbinu ya usimulizi wa kimonolojia kuakisi dhamira ya maadili kwa kukemea tabia ya wizi katika jamii. Anatumia viambishi vya nafsi ya kwanza umoja kama 'na' katika neno *naanza*, 'ni' katika neno *ninayosema*, *nilinenewa* na 'si' katika neno *sijikawizi.* Viambishi hivi vinaibua mtindo wa usimulizi wa kimonolojia unaowasilisha hisia binafsi. Mwandishi anadhihirisha hilo kwa kusema:

1. **Nazileta simulizi, mbele yenu wanadama**
*Na*anza *si*jikawizi, sikia *ni*nayosema
Nilinenewa upuzi, naye alokuja hima
Niaye sikumaizi, anena bila kupima
Kapatwa na bumbuwazi, aliponijua vyema
Mwanadamu huyanena, yajazayo moyo wake.

2. Nikiwa na simu yangu, **siku moja mtaani**
Akashuku mlimwengu, ni ya kwake akidhani
Akapiga yowe kwangu, **mwizi** eh! **mwizi!** jamani
Wameshashika marungu, wakasema ipigeni
Kumbe ya kwake mwenzangu, imo mwake mfukoni
Mwanadamu huyanena, yajazayo moyo wake.
(uk. 24)

Katika dondoo hili, maswali kadhaa kuhusu wizi yanazuka: Kwa nini wizi unaonekana kuwa kitendo kibaya na nani amehalalisha kuwa si tendo jema? Mtazamo wa kiteolojia unaeleza kuwa haki ya kumiliki mali ni msingi wa maadili na sheria nyingi (Cruft, 2022). Wizi ni uvunjaji wa msingi huu kwa sababu unahusisha kuchukua mali ya mwingine bila idhini. Maamuzi ya mwanadamu hutegemea akili, utambuzi, na uhuru, misingi inayosimamia matendo yake. Borges (2021), akimrejelea Kant (1881), anaona mwanadamu kama wakala wa maadili anayeweza kutumia akili, utambuzi na uhuru kuamua bila kuathiriwa na matokeo ya nje. Kwa hivyo, kupitia

usimulizi, mwandishi ameibua dhamira ya maadili yenye vipengele vitatu; akili, utambuzi, na uhuru vinavyoonesha Nguvu Asili iliyomo ndani ya mwanadamu.

### 4.2.2 Usimulizi wa Kidayalojia

Mbinu hii ya usimulizi wa kidayalojia imebainika kupitia msingi wa kwanza wa Nadharia ya Umtindo kama tulivyoeleza katika kipengele cha 4.2.1. Hivyo, katika diwani ya *Ngonjera Zetu 1* (2020), waandishi wanatumia mtindo wa dayalojia kama kipengele cha kifani kinachoakisi dhamira ya toba na msamaha. Mtindo wa dayalojia baina ya wahusika husaidia kuonesha tofauti za kimtazamo na uhalisia wa mambo katika jamii. Katika shairi la 'Kubeti' waandishi wanaibua mjadala mzito kuhusu suala la kubeti kama ifuatavyo:

7. MFAUME
Hivi sasa nimejua, mie nishazindukana,
Baada ya kuchambua, sijaona la maana,
Ndipo nilipoamua, **kubeti tena Hapana**,
Sithubutu.

8. ULAMAA
Umefanya ujasiri, kuikataa kamari,
Hayo mawazo mazuri, kurudia ni kiburi,
**Akusamehe Kahari**, ya siri na dhahiri,
Omba dua.

9. MFAUME
Nashukuru ndugu yangu, **Mungu anisaidie**,
**Apokee dua zangu**, na **toba aitikie**,
Pamoja nao wenzangu, Kamari tuikimbie,
Tuongoke.

10. ULAMAA
Kubeti sio ajira, hongera kwa kuelewa,
Uamuzi wa busara, huo ulouchukuwa,
Umekutoka ujura, sasa umekuwa sawa,
Aamin.
(uk. 22)

Kwa mujibu wa shairi husika, waandishi wanakemea mchezo wa kubeti wakieleza kuwa ni kinyume na maadili yanayomtaka mtu kufanya kazi halali. Wanatoa wito kwa wanajamii kuacha tabia hiyo ili kuepuka adhabu kutoka kwa Nguvu Asili zilizoweka kanuni hizo. Hili linaendana na msingi wa nne wa Nadharia ya Udhanaishi

unaosisitiza kuwa licha ya uhuru wake, mwanadamu anawajibika kwa matokeo ya maamuzi yake. Kupitia mtindo wa **dayalojia**, waandishi wanaibua dhamira ya **toba na msamaha**.

Dhamira ya toba na msamaha si jambo jipya katika fasihi ya Kiswahili, kwani wachambuzi kama Ngunyi (2017) na Odhiambo na Mutiso (2021) wameijadili kwa kuhusisha na dini, ingawa ni dhamira ya kiteolojia katika tawi la eskatolojia. Katika shairi husika, wahusika wanadhihirisha uhusiano wao na Nguvu Asili. Mathalani, Mfaume anakiri kosa lake la kubeti na kuamua kuacha, hatua muhimu ya katika mchakato wa toba. Ulamaa, akitambua uzito wa kosa hilo, anasaidia kurejesha uhusiano kati ya Mfaume na Nguvu Asili na kumwelekeza njia ya kuepuka hukumu ya baadaye. Hivyo, toba na msamaha huonekana kama nyenzo za kupata rehema na kupunguza adhabu ya baadaye.

Dhamira ya toba na msamaha inajitokeza pia hata katika diwani ya *Wino wa Kalamu Ndogo* kupitia mtindo wa usimulizi wa kidayalojia. Mwandishi anavaa uhusika wa baba kutoa wosia kwa mwanawe kama anavyosema katika shairi la ‘Utenzi wa Baba kwa Mwana’ katika uk. 56:

83 Mwenza akikukosea
Ama ukimkosea
Ni vyema mkaongea
Suluhu mkafikia.

84. Atawaridhia Baba
Na kujazika vibaba
Mtakula na kushiba
Vifungo vitaachia.

Katika dondoo hili mwandishi anasema, “Mwenza akikukosea, Ama ukimkosea, Ni vyema mkaongea, Suluhu mkafikia.” Uteuzi wa msamiati katika vipande hivi vinaonesha hisia na wito wa huruma na msamaha kwa pande zote mbili. Baba, kama mhusika, anamshauri mwana kuwa ikitokea amekosewa na mwingine, au yeye mwenyewe ikitokea amekosea, ni muhimu kuzungumza na kutafuta suluhu. Kwa hivyo, kupitia vipande hivi, dhamira ya huruma na msamaha inasisitizwa. Mwandishi anaonesha kuwa makosa ni sehemu ya maisha, na ni vyema kutafuta maridhiano ili kuepuka hasira au chuki. Huruma na msamaha ni mbinu bora ya kupunguza migogoro na kuleta suluhu, kama anavyoeleza baba (mzazi). Katika jamii, msamaha ni nguzo muhimu katika uhusiano wa kifamilia. Mwandishi anaendelea kusema, “Ni vyema mkaongea” ili kumaanisha kwamba, hata wale wanaokosea wanahitaji kuelewana na

kuzungumza na wale waliokosewa ili kufikia msamaha. Huruma inajitokeza kwa kumfundisha mwana kuwa kila mtu anaweza kukosea; hivyo, ni muhimu kuwahurumia wale wanaoomba msamaha badala ya kuwahukumu.

Vilevile, mwandishi anatumia neno Baba kurejelea **Nguvu Asili**, akimwonesha kama chanzo cha **msamaha, neema na baraka** kwa wale wanaoonyesha huruma kwa wengine. Kauli kama "Atawaridhia Baba" na "kujaza vibaba" zinaashiria kuwa msamaha huleta mafanikio na utulivu wa kifamilia. Dhamira ya **huruma na msamaha** inaendelea kuimarishwa kupitia mistari kama "Mtakula na kushiba, Vifungo vitaachia", inayoonesha kuwa kutoa msamaha huleta amani, faraja na ufanisi wa maisha kwa jamii na familia.

## 4.3 Matumizi ya Lugha

Kipengele hiki kimebainika kupitia Nadharia ya Umtindo, ambayo inasisitiza kuwa uhakiki wa matini za kifasihi unahusisha vipengele vya lugha vinavyojenga dhana mbalimbali za kifani kama maana msingi, maana fiche, urari, ulinganifu, ukiushi wa kanuni, tamathali za semi, mandhari, taswira, vielelezo, ishara na kile kinachoashiriwa (Barry, 2002). Kwa msingi huo, matumizi ya lugha katika ushairi ni ya msingi kwa kuwa huleta mvuto na kuibua hisia mbalimbali kwa hadhira. Aidha, nadharia hii inaeleza kuwa lugha hutumika kama chombo cha kubeba na kuakisi maudhui ya kazi ya kifasihi.

### 4.3.1 Uteuzi wa Msamiati

Uteuzi sahihi wa msamiati pamoja na tamathali za semi, mpangilio wa maneno na mbinu nyingine za kisanaa ni muhimu katika ufanisi wa kazi ya fasihi kwani huakisi dhamira mbalimbali (Njogu na Chimerah, 1999). Katika shairi la *'Malenga wa Mvita'*, matumizi ya lugha, hasusani uteuzi wa msamiati, yanaunganisha mawazo ya waandishi na mwitikio wa wasomaji. Suala hili linaendana na msingi wa pili wa Nadharia ya Umtindo unaosema kuwa vipengele vya lugha humpa mwandishi chaguzi nyingi za kuwasilisha mawazo yake. Kupitia msingi huu tumechunguza muktadha wa matumizi ya maneno husika katika kubaini ukweli unaofumbatwa katika matini. Muktadha wa kijamii unajitokeza kupitia uteuzi wa msamiati unaorejelea kifo kama tukio la kijamii. Hisia, tafakuri, pamoja na hamasa anayoipata msomaji au msikilizaji ni matokeo ya uteuzi mzuri wa msamiati kama inavyojibainisha katika dondoo lifuatalo:

2. MFAUME
Sijui pa kuanzia, **machozi yatiririka**,
Bado ninafikiria, **hivi kweli katutoka**?

Mengi ametufanyia, mpaka hapa kufika,
**Moyoni ninaumia**, **muda wote ninaweza**.

83. MFAUME
Habari niliyopata, yafanya nasawajika,
Inanifanya nadata, akili yatatizika,
**Msiba umetukuta**, Waswahili kwa hakika,
Ni malenga wa Mvita, **ndugu yetu katutoka**.
(uk. 100)

Katika dondoo hili maneno yanayoibua hisia za majonzi na huzuni (machozi yatiririka, hivi kweli katutoka, moyoni ninaumia, muda wote ninaweza, msiba umetukuta, ndugu yetu katutoka) yameteuliwa kwa lengo la kuasiki dhamira ya kifo. Neno 'machozi' (ubeti wa 2 mshororo wa 1 kipande cha 2) ni nomino inayoashiria matokeo ya maumivu ya mwili au mahangaiko ya nafsi. Pia, 'msiba' (ubeti wa 4 mshororo wa 3 kipande cha 1) ni nomino inayorejelea muktadha wa kijamii unaohusisha tukio la hisia za majonzi. Kadhalika, neno 'ninaumia' (ubeti wa 2 mshororo wa 4 kipande cha 1) na neno 'umetukuta' (ubeti 4 mshororo wa 3 kipande cha 1) pamoja na neno 'katutoka' (ubeti wa 4 mshororo wa 4 kipande cha 2) ni vitenzi vinavyorejelea hisia za majonzi kwa mtu au jamii iliyompoteza mpendwa wao.

Dhamira ya kifo katika dondoo hili ni ya kiteolojia inayohusiana na Nguvu Asili. Kifo kinaelezwa kama tukio lisisilodhibitika, linaloleta maumivu, msiba, na mabadiliko yanayoathiri maisha ya binadamu, na jinsi wanavyoshughulika na Nguvu Asili zinazozunguka maisha yao. Katika dondoo hii, Mfaume anasumbuliwa na fikra za kuondokewa na malenga wa Mvita. Maumivu ya msiba yanaonekana kama kipengele cha asili kilichoshindwa kudhibitiwa. Hali hii inajidhihirisha katika ubeti wa 2 mshororo wa 4 pale anaposema 'Moyoni ninaumia, muda wote ninaweza.' Aidha, matokeo ya utaratibu wa Nguvu Asili ni uthibitisho wa namna nguvu hiyo inavyoathiri maisha ya binadamu kiasi cha kusababisha maumivu na huzuni. Hali ya majonzi na huzuni imeelezwa pia katika msingi wa tano wa Nadharia ya Udhanaishi kuwa katika maisha ya mwanadamu, kuna upande wa giza unaomnyima utulivu wa kifikra na kiroho. Upande wa giza unaodokezwa na msingi huu ni kifo. Kadhalika, kifo, kama dhamira ya kiteolojia, kinajitokeza kwa jinsi Mfaume anavyokubaliana na hali halisi ya msiba unaotokea. Uteuzi wa maneno kama "machozi yatiririka" na "moyoni ninaumia" unaonesha uhusiano wa binadamu na maumbile ambapo maumivu na msiba ni sehemu ya mzunguko wa asili wa maisha. Maumivu yanayoletwa na msiba ni sehemu ya mfumo wa Nguvu Asili, ambapo mabadiliko katika hali ya binadamu (kama kifo au kuondokewa na mtu wa karibu) ni matokeo ya Nguvu Asili zinazosimamia maisha.

Katika shairi hili, ingawa dini hujitokeza kupitia tamaduni za kijamii na maadili yanayohusiana na kifo, **teolojia inayoangazia Nguvu Asili** inaonekana wazi katika jinsi binadamu anavyokabiliana na msiba na maumivu **bila kumtegemea Mungu au imani za kidini**. Hali hii inaonesha kuwa teolojia, kama mjadala wa **Nguvu Asili,** inahusiana na maumbile, maumivu, huzuni na mabadiliko yanayotokana na mfumo wa asili unaoongoza maisha (Madden, 2021). Hivyo, **maumivu na msiba** vinaelezwa si kama adhabu au matokeo ya mapenzi ya Mungu, bali kama sehemu ya mzunguko wa kimaumbile unaoathiri maisha ya binadamu.

### 83.3.2 Matumizi ya Methali

Nadharia ya Umtindo inaeleza kwamba, kwa kuwa fasihi huwasilishwa kupitia lugha, matini za kifasihi haziwezi kuepuka viwango vya umtindo vinavyohusika na isimu. Viwango hivyo ni pamoja na grafolojia, fonolojia, leksikolojia, sintaksia, semiolojia, semantiki na pragmatiki. Mtunzi anatumia kiwango cha sintaksia sambamba na kiwango cha semiolojia kuibua methali zilizobeba dhamira aliyokusuda. Katika kiwango cha sintaksia uteuzi wa kategoria ya maneno aina ya vishazi tegemezi umesaidia kuunda methali isemayo '**Aupendaye uzee,** hatozichukia mvi.' Pia, kiwango cha semiolojia kilichotumika kinajihusisha na alama na ishara katika kuunda methali zisemazo 'Kama wautaka **moto**, ujiandae kwa **jivu**.' Mtunzi anatumia ishara za usababisho kuonesha ufungamano wa kiusababishani kati ya ishara (jivu) na kinachoashiriwa (moto). Tutachunguza zaidi katika dondoo husika baada ya ufafanuzi wa dhana ya methali kulingana na baadhi wa wataalamu.

Wataalamu mbalimbali wa tafiti zinazohusu masuala ya paremiolojia[6] kama Daniel (1987) na Wamitila (2003), wanaona kuwa jukumu kubwa la methali katika fasihi ni kupitisha mawaidha yanayolenga kuasa au kushauri jamii kuhusu maisha kwa ujumla. Pia, wanaeleza kuwa methali zinaweza kusaidia kufasiri maisha yetu ya kale, ya sasa, na hata yajayo. Sambamba na kufasiri maisha ya jamii katika vipindi mbalimbali, pia, huakisi yale yaliyomo katika jamii. Vivyo hivyo, hata zinapotumika kwenye matini za ushairi hufasiri na kuakisi maudhui yaliyokusudiwa na mwandishi. Suala hili linajidhihirisha vizuri katika diwani ya *Wino wa Kalamu Ndogo* kupitia shairi la 'Mwogopa Kasoro'. Mwandishi anasema:

> Washangaza si kidogo, kwa haya unayofanya
> Kung'atang'ata kisogo, ukipuliza ja panya

---

[6] Paremiolojia ni taaluma inayojishughulisha na uchunguzi na uchambuzi na ufasiri wa methali, misemo, mafumbo, mifano na vielelezo katika muktadha wa kifasihi (Nortojeva, 2024).

**Aupendaye uzee, hatozichukia mvi**

**Kama wautaka moto, ujiandae kwa jivu**
Waupingaje msoto, na wataka ushupavu
**Aupendaye uzee, hatozichukia mvi**

Vizuri vya kutajika, pia huwa na dosari
Hilo lisikupe shaka, mia hubeba sifuri
**Aupendaye uzee, hatozichukia mvi**
(uk. 36)

Katika dondoo hili mwandishi anatumia kibwagizo chenye methali isemayo, "Aupendaye uzee, hatozichukia mvi" kama mojawapo ya kipengele cha kifani katika matumizi ya lugha kuakisi dhamira ya kukubali matokeo. Methali hii imeundwa na kishazi tegemezi kinachohitaji kukamilishwa na kishazi kingine katika upande wa pili. Methali nyingine iliyojitokeza ni "Kama wautaka **moto**, ujiandae kwa **jivu**." Methali hii pamoja na ile ya "Aupendaye **uzee**, hatozichukia **mvi**" zote zimejengwa kupitia ishara za usababisho ambapo 'mvi' huashiria 'uzee' kadiri ya muktadha wa kijamii na 'jivu' huashiria 'moto'. Methali hizi zinarejelea dhamira moja inayodhihirisha uumbaji katika tawi la anthropolojia. Kwa kurejelea muktadha wa kijamii, kama Nadharia ya Udhanaishi inavyodai kuwa uwepo ulitanguliwa na kutokuwepo; vivyo hivyo, mwandishi anaonesha kuwa katika maisha kuna mwanzo na mwisho wa kila kitu. Jambo la msingi ni kukubali matokeo, yawe mazuri au mabaya. Mwandishi anaonesha kuwa mabadiliko ya kimwili ni sehemu ya uumbaji unaoratibiwa na Nguvu Asili, nguvu zipitazo kila nguvu. Taswira ya mvi, mbali na kuashiria uzee, inajitokeza kama sehemu ya uumbaji ambayo haiwezi kuepukika. Hivyo, haina budi kupokelewa tu kama sehemu ya taratibu na kanuni za mpango wa Nguvu Asili; hakuna sababu ya kupambana na uhalisia (uzee) kwani ni sawa na kufukuza upepo kwa maana kila kitu kimesharatibiwa.

### 83.3.3 Matumizi ya Misemo

Watunzi wametumia usambamba wa kifahiwa ili kuibua kipengele cha misemo inayorejelea dhamira ileile. Usambamba huu unajibainisha pindi fahiwa moja inaporudiwa na huku mtunzi akiendelea kutumia muundo wa sentensi unaolandana. Msingi wa tatu wa Nadharia ya Umtindo unasisitiza uwezekano wa watunzi kutumia kipengele fulani cha lugha kulingana na ufaafu wake kwa dhamira, wazo, ujumbe au hali husika. Kipengele cha lugha kinacholeta usambamba wa kifahiwa ni kategoria ya maneno aina ya virai nomino yaliyotumika katika shairi la 'Jeuri' kama tutakavyojadili baada ya ufafanuzi wa dhana ya misemo.

Misemo ni tungo fupi za kisanaa zinazotumia tamathali, lugha ya picha, ishara na vielelezo ili kuunda taswira ya hali, tukio, au wazo kwa njia ya kiufundi (King'ei na Ndalu, 2007). Huibuka katika muktadha wa kijamii na kimaadili kwa malengo maalum, kisha huenea katika jamii, na baadaye hubadilika, kutoweka au kudumu kwa muda mrefu katika kumbukumbu za jamii (Mulokozi, 2017). Hemed na Hamisi (2020) wanaeleza kuwa misemo huakisi hali mbalimbali za kijamii, kama inavyoonekana katika mashairi yao 'Jeuri' na 'Ni Sasa sio Baadaye'. Katika shairi la 'Jeuri' linaonesha mtindo wa majibizano baina ya wahusika kama ifuatavyo:

1. ULAMAA
   **Dunia hii duara**, ni vema tuwe makini,
   Ina nema na madhara, watu wema na wahuni,
   Vema tuwe na subira, tajiri na masikini,
   *Sitofanya ujeuri*, **dunia rangirangile**.

2. MFAUME
   **Dunia rangirangile**, hata mimi ninajuwa,
   Aso hili ana lile, mara nyingi hivyo huwa,
   Ukifanya upotole, rangize utang'amuwa,
   *Sitoifanya jeuri*, **dunia tambara bovu**.

3. **Dunia tambara bovu**, ina nyingi changamoto,
   Vipi ufanye maovu, wakati hapa mapito,
   Si pekee mwenye nguvu, kijana, mama, mtoto,
   Sitoifanya jeuri, **dunia mti mkavu**.

4. **Dunia mti mkavu**, hilo kweli nasadiki,
   Haihitaji utovu, wengine kuwadhihaki,
   Yahitaji utulivu, kuishi katika haki,
   *Sitoifanya jeuri*, **dunia mwendo wa ngisi**.

5. **Dunia mwendo wa ngisi**, ya nini kujifutua,
   Ujione almasi, thamani kuichukua,
   Imejaa ukakasi, kama kuni za mabua,
   *Sitoifanya jeuri*, **dunia sawa kikongwe**.
   (uk. 109)

Katika beti hizi, kuna misemo kadhaa kama "dunia hii duara," "dunia rangirangile," "Aso hili ana lile," "dunia tambara bovu," "dunia mti mkavu," na "dunia mwendo wa ngisi," ambayo imeundwa kwa kutumia virai nomino ambapo neno dunia ndilo neno kuu. Misemo hii inaonyesha jinsi jamii inavyoitazama dunia katika mambo mbalimbali. Aidha, misemo hiyo ina sifa ya kufumbata sitiari, ambapo waandishi wanatumia hali, vitu au matukio yaliyowazunguka, waliyoshuhudia au kusimuliwa ili kuakisi maudhui ya kazi yao (Mosha, 2022). Pia, dhana ya usambamba wa kifahiwa

inaonekana katika misemo mbalimbali kama ‘dunia hii duara,’ ‘dunia rangirangile,’ ‘dunia tambara bovu,’ ‘dunia mti mkavu,’ na ‘dunia mwendo wa ngisi,’ zote zikirejelea maana moja kwamba dunia ina mambo mema na mabaya, na mwanadamu anapaswa kuwa makini. Pia, kuna uchimuzi wa anafora ambapo sehemu ya mshororo wa mwisho hutumika kama mwanzo wa mshororo wa kwanza katika ubeti unaofuata, ili kuendeleza wazo au hoja katika shairi. Misemo mingine pia inaonekana katika shairi la ‘Ni Sasa sio Baadaye’ kama ifuatavyo:

1. ULAMAA
   **Zama zinabadilika** hakuna anayebisha
   Yanakuja yaondoka, yanayoanza yanakwisha,
   Mipango uloiweka, fanya kwa kuharakisha
   **Muda ni huu wa sasa**, wala sio baadaye.

2. MFAUME
   Jitahidi fanya hima, **muda haukusubiri**,
   Zitimize zako dhima, utakayo yanawiri,
   **Nenda mzimamzima**, huku ukitafakari,
   **Muda mzuri ni sasa**, baadaye huijui.
   (uk. 107)

Kupitia beti hizi waandishi wanaibua misemo kama “zama zinabadilika (usiishi kwa mazoea) muda ni huu wa sasa (muda ni mali), muda haukusubiri (muda hauendi nyuma), nenda mzimamzima (nenda kwa ukamilifu), na muda mzuri ni sasa (kila jambo na wakati wake).” Aidha, katika madondoo haya mawili ya beti hizo tumebaini kuwa sitiari pamoja na misemo iliyojitokeza inaakisi dhahiri dhamira ya neema katika anthropolojia kama tawi mojawapo la teolojia.

Kwa mujibu wa O’Donoghue (1957), neema ni zawadi inayotolewa bila juhudi kutoka kwa mpokeaji, bali kama mpango wa Nguvu Asili. Mtazamo huu unaakisiwa katika shairi la Ni Sasa sio Baadaye ambapo waandishi wanasema, “Yanakuja yaondoka, yanayoanza yanakwisha,” wakionyesha kuwa mambo hutokea kwa mpango wa asili usioegemea juhudi za binafsi. Vilevile, katika shairi la Jeuri, waandishi wanasema, “Vema tuwe na subira, tajiri na masikini,” wakisisitiza uvumilivu katika hali yoyote, kwa kuzingatia kuwa mambo mengi hayaamuliwi na mwanadamu. Kupitia nukuu hizi, neema inajitokeza kama zawadi. Inatazamwa kama hiari ambayo ipo nje ya udhibiti wa kibinadamu, na humnufaisha mpokeaji bila juhudi au matarajio yoyote kama malipo. Waandishi wanaonesha kuwa mabadiliko ya zama yako nje ya uwezo wa kibinadamu. Mtazamo huu unasawiri Nadharia ya Udhanaishi katika msingi wake wa pili unaodai kuwa imani kwa Mungu (nguvu zipitazo kila nguvu) ndio msingi wa maana ya maisha vinginevyo maisha hayana maana. Kwa mantiki hiyo, ni dhahiri kuwa ili maisha yawe na maana, mwanadamu anapaswa kuacha kutegemea dunia;

badala yake, ategemee nguvu zilizo juu ya uwezo wake. Katika kutumainia nguvu hizo neema humshukia kama mvua. Mwandishi anahoji, ‘vipi ufanye maovu, wakati hapa mapito’. Neno ‘mapito’ na ‘dunia hii duara’ yanarejelea hali ya mzunguko au mjongeo, hivyo, ni lazima mwanadamu ajihadhari kwa maana katika mzunguko, dunia huleta vyema na vimbi. Tukirejelea madondoo yote mawili tunaweza kukiri kwamba, waandishi wanaonesha kuwa wana utambuzi wa kutosha kuhusu changamoto za mabadiliko ya nyakati ndio maana wanathubutu kuikumbusha jamii kuhusu mabadiliko hayo. Kadhalika, katika mjadala wa kiteolojia, neema pia hutazamwa kama stahiki au tuzo inayohusisha juhudi za kibinadamu katika kuipata au kupoikea (Pohle, 2009). Kwa mfano, katika shairi la ‘Jeuri’, waandishi wanasema, “Yahitaji utulivu, kuishi katika haki”, “Sitoifanya jeuri, dunia tambara bovu.” Nukuu hizi zinaonesha kuwa aina hii ya pili ya neema haitokani na mtiririko wa asili wa matukio au ushawishi wa nguvu ya nje, kama vile utendaji kazi wa asili, wakati au mazingira (Kho, 2021).

Katika muktadha wa kiteolojia, neema inaweza pia kueleweka kama dhana ambayo mtu hunufaika kutokana na juhudi binafsi na hali au nguvu za nje (kama asili, bahati nasibu, au mifumo ya kijamii) ambayo ipo nje ya uwezo wa binadamu, na mara nyingi kwa njia ambazo haziwezi kutabiriwa au kueleweka kikamilifu (Scheeben, 2024). Ndio maana washairi wanasisitiza kuwa ‘yahitaji utulivu, kuishi katika haki’. Huu ni wajibu ambao mwanadamu anapaswa kuutekeleza ili aweze kupata neema kama tuzo kutokana na uwajibikaji wake.

**83.4 Mandhari**

Waandishi wa diwani teule wamejenga mandhari inayodokeza mazingira ya porini na kijijini kupitia kiwango cha kisintakisia. Wameteua maneno ya kategoria ya nomino yanayohusiana na mazingira wanayoyawasilisha ili kuibua dhamira waliyokusudia. Mathalani, uteuzi wa nomino kama vile ‘miti’ na ‘misitu’ hujenga picha ya mazingira tengefu ya hifadhi kwa ajili ya maliasili kama itanavyodhihirika kwenye shairi la ‘Mti’ tutakalodondoa baadaye.

Mandhari ni kipengele muhimu cha kifani chenye uhusiano wa karibu na mazingira ya asili, hali ya hewa, au mazingira ya kijamii na kiutamaduni, ambacho hutumika katika fasihi ili kuunda muktadha wa kihisia na kifikra. Mandhari huchangia katika kuwasilisha maudhui kwa hadhira kwa njia ya kuvutia (Bulaya, 2016). Kwa kawaida, hujumuisha vipengele kama maumbile, hali ya hewa, miji, vijiji, na hali za kijamii au kisiasa ambazo huimarisha au kusaidia kuelewa maudhui ya kazi. Waandishi Hemed na Hamisi (2020) wamaefanikiwa kutumia nomino zinazowakilisha picha za mandhari

kujenga hisia na fikra kuhusu utunzaji wa mazingira, kama inavyoonekana katika shairi lao 'Mti':

1. ULAMAA (Mwanakijiji)
   Bora tuchome **mkaa**, kuyakidhi mahitaji
   **Miti** imetapakaa, kila pembe ya kijiji
   Haileti manufaa, bora tufanye mtaji.

2. MFAUME (Afisamisitu)
   Ni mawazo ya kutingwa, fikiria mara mbili,
   Utasababisha **jangwa**, kwa hiyo yako akili
   Ni lazima utapigwa, tambua huu ukweli.

4. Yakupasa kutambuwa, umuhimu wa **misitu**,
   Husababisha mvuwa, kwenye maeneo yetu,
   Na unyevu mwingi huwa, **ukame** usiwe katu.

6. **Misitu** chanzo cha maji, tunachokitegemea,
   Yahitaji utunzaji kuweza kukitetea,
   Msifanye ufujaji, **miti** itateketea.

8. Hatuhitaji makofi, kuweza eleweshana,
   **Miti** ndiyo malighafi, itupavyo vya maana,
   Mvua na hewa safi, kwenye **miti** hutokana.

9. ULAMAA (Mwanakijiji)
   Sasa nimeshaamini, kwa kweli mnatupenda,
   **Miti** nitaithamini, sitakata nitapanda,
   Shoka naliweka chini, kuikata sitaenda.
   (uk. 29)

Waandishi wametumia mandhari kama kipengele cha kifani kuakisi dhamira ya utunzaji wa mazingira ambayo ina uhusiano mkubwa na masuala ya uumbaji katika anthropolojia kama tawi mojawapo la teolojia. Waandishi wanataja mambo asilia yenye uhusiano na Nguvu Asili kama vile misitu, maji, hewa, unyevu, na mvua. Vitu vyote hivi vinajenga dhamira ya kiteolojia ya utunzaji mazingira kama mkakati wa kuendeleza uhai unaosisitizwa na msingi wa tatu wa Nadharia ya Udhanaishi. Msingi huu unadai kuwa, mwanadamu husukumwa kutekeleza matakwa ya nguvu zilizomuumba katika kutii kanuni za kimaadili zilizowekwa na nguvu hizo. Kwa hiyo, suala la kuheshimu, kutunza na kulinda uhai ni suala la kimaadili linaloratibiwa na nguvu zilizo juu ya uwezo wa mwanadamu ambazo humsukuma kutekeleza mpango huo. Pamoja na hayo, waandishi wanaibua pia dhana ya usambamba wa kidhamira kupitia nomino kama miti, misitu, mkaa, jangwa na ukame. Wamitila (2008) anaeleza kuwa aghalabu usambamba wa kidhamira hudhihirika katika mazingira ambayo wazo

linaloongelewa linarudiwa. Kwa hiyo, nomino tulizobainisha, kimsingi, zina uhusiano fulani wa kimantiki unaobeba wazo moja licha ya kwamba zinatofautiana. Wazo kuu linajidhihirisha kupitia nomino hizo ni utunzaji wa mazingira.

Dhamira ya utunzaji wa mazingira katika muktadha wa kiteolojia inazingatia Nguvu Asili zinazoshughulikia uhusiano wa binadamu na ulimwengu wake, pasipo kuihusisha na imani za kidini. Nguvu asili, kama vile mzunguko wa maji, mvua, na mabadiliko ya viumbe hai, zinatengeneza mfumo wa kimazingira unaoshikilia usawa wa dunia, na binadamu anapaswa kutunza na kuheshimu mfumo huu. Hivyo, utunzaji wa mazingira ni jukumu la kijamii na kimazingira linalotokana na kutambua, na kuheshimu Nguvu Asili za ulimwengu, bila kumuhusisha Mungu au miungu kama chanzo cha nguvu hizo. Shiva (2005) anasisitiza kuwa utunzaji wa mazingira ni haki ya asili ya kila kiumbe, na hivyo, ni wajibu wa binadamu. Kadhalika, waandishi nao wamedhihirisha hilo kupitia shairi lao la 'Mti'.

Kwa mujibu wa Berry (2009) na Haught (2012), dunia na mazingira yake ni sehemu ya mfumo wa Nguvu Asili unaoendelea na unaostahili kuheshimiwa. Binadamu wanapaswa kuelewa uhusiano wao na dunia, wakitazama uumbaji si tu kama chanzo cha kimungu bali pia kama sehemu ya Nguvu Asili zinazopaswa kulindwa. Mawazo haya yanatofautiana na ya kidini, ambapo utunzaji wa mazingira hutokana na imani katika Mungu au miungu kama chanzo cha nguvu hizo. Katika muktadha wa teolojia, utunzaji wa mazingira kama ilivyo katika mtindo wa Nguvu Asili, hautegemei imani ya kidini au hadithi za kidini za uumbaji, bali inazingatia mifumo ya asili inayosimamia maisha na mzunguko wa viumbe hai. Mathalani, katika shairi la 'Miti' Afisamisitu na Mwanakijiji wanadhihirisha kuwa utunzaji wa misitu ni sehemu ya kuelewa na kuheshimu mfumo wa asili, unaoshikilia usawa wa maumbile, na sio amri za kidini.

## 5.0 Hitimisho

Makala haya yamejadili vipengele vya kifani vinavyoakisi dhamira za kiteolojia katika ushairi andishi wa Kiswahili. Miongoni mwa vipengele vya kifani vilivyobainika kuakisi dhamira za kiteolojia katika ushairi andishi wa Kiswahili, kwa kuzingatia diwani teule, ni pamoja na taswira, mtindo wa usimulizi (monolojia na dayalojia), matumizi ya lugha (uteuzi wa msamiati, methali na misemo), pamoja na mandhari. Matokeo yanaonesha kuwa vipengele vya kifani vilivyotumiwa na waandishi Elenzian Komba pamoja na Ulamaa Hemed na Mfaume Hamisi katika diwani zao vimefumbata dhamira za kiteolojia ambazo ni pamoja na utamaduni, matendo mema, toba na msamaha, kifo, kukubali matokeo, neema na utunzaji wa mazingira. Makala haya yameongeza maarifa katika ushairi wa Kiswahili kwa

kutambulisha vipengele vya kifani vinavyoakisi dhamira za kiteolojia katika ushairi andishi wa Kiswahili tofauti na mitazamo inayohusisha dhamira za kiteolojia na masuala ya kidini katika ushairi andishi wa Kiswahili.

## Marejeleo

Ammon, U. (Mh.) (1989) *Status and Function of Languages and Language Varieties.* Boston: De Gruyter.

Barry, P. (2002) *Beginning Theory: An Introduction to Literary and Cultural Theory.* Manchester: Manchester University Press.

Berry, J. (2023) "Aquinas's Understanding of Religion". *Religions*. Juz. 14(7):1-16. https://doi.org/10.3390/rel14070855

Bora, M.J. (2020) "Reflection of Existentialism in Albert Camus the Outsider". *International Journal of Management and Humanities*, Juz. *5*(2): 1-3. https://www.ijmh.org/wp-content/uploads/papers/v5i2/B1139105220.pdf

Borges, M. (2021) *Emotion, Reason, and Action in Kant*. Great Britain. Bloomsbury Publishing Plc.

Bulaya, J. (2016) *Mandhari na Usawiri wa Ukimwi katika Riwaya ya Kiswahili 2000-2010*. Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Calloway, K. (2023) *Literature and Natural Theology in Early Modern England*. Cambridge: Cambridge University Press. https://doi.org/10.1017/9781009415231

Camus, A. (1984) *The Myth of Sisyphus, and Other Essays*. London: Penguin.

Carter, M. J. na Carter S. (2024) "How Themes in Literature Can Inform Sociological Theory, Research, and Teaching". *The American Sociologist* Juz. 45(4): 388-411 DOI:10.1007/s12108-014-9221-1

Croitoru, I. M. (2020) Theology and Science in Dialogue. Signposts and Perspectives. *International Journal of Theology, Philosophy and Science*, Juz. 4(7): 39-61.

Crosby, D. (2022) "Augustine's Confessions". *The Classical Review*, Juz. 72(2): 562–564. https://doi.org/10.1017/S0009840X22000956.

Cruft, R. (2022) "On Rights, Human Rights, and Property: A Response." *Journal of Applied Philosophy*, Juz. 39(2): 220-232. https://doi.org/10.1111/japp.12507.\

Daniel, J.L. (1978) Towards an Ethnography of Afro-American Proverbial Usage. *Black Lines 2* Na. 4: 3-12.

Durkheim, E. (2001) *The Elementary Forms of Religious Life*. New York: Oxford University Press.

Eikelboom, L. (2022) “Reading for Form in Doctrine: Literary Approaches to Przywara’s Analogia Entis”. *The Journal of Religion*, Juz. 102: 307-331. https://doi.org/10.1086/719824.

Falconer, R. (2019) *Hell in Contemporary Literature: Western Descent Narratives Since 1945*. Edinburgh. University Press.

Huneeus, C. (2025) “The functions of Natural Theology in Thomas Aquinas: A Presumption of Atheism?” *Religious Studies*, Juz. 61(1): 152–165. https://doi.org/10.1017/S0034412523000616

Kho, Y. (2021) “Meritorious Heroes. Sungkyun”. *Journal of East Asia Studies*, Juz. 21(1): 1–25 DOI: Org/10.1215/15982661-8873872.

Kierkegaard, S. (1974) *Concluding Unscientific Postscript*. Princeton: Princeton University Press.

Kinara, G., Ngugi, P. M. Y. na Wafula, R. M. (2024) “Mapokeo ya Utenzi wa Mwana Kupona katika Upya wa Shaaban Robert: ‘Utenzi wa Hati’ na ‘Utenzi wa Adili’.” *East African Journal of Swahili Studies,* Juz. 7(1): 319-331. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2043.

King'ei, K. na Ndalu A. (2007) *Kamusi ya Semi* (Toleo Jipya). Nairobi: East African Educational Publishers.

Kress, G., na Van Leeuwen, T. (2020) *Reading Images: The Grammar of Visual Design*. London: Rotledge.

Leech, G. (1969) *A Linguistic Guide to English Poetry,* London: Longman Group Ltd.

Leech, G.N. na Short, M.A. (1981) *Style in Fiction: A linguistic Introduction to English Fictional Prose*. London: Longman Group Limited.

Leech, G. (2008) *Language in Literature: Style and Foregrounding.* Harlow: Pearson Longman.

Lodhi, A. (2010) *Teolojia ya Fasihi ya Kiswahili: Maadili na Dini.* Nairobi: Oxford University Press.

Madden, J. (2021) “The Evolution of Suffering, Epiphenomenalism, and the Phenomena of Life: Evidential Problems for Naturalists”. *Religions*, Juz. 12(9):1-14.https://doi.org/10.3390/rel12090687.

Malugu, A. (2016) “Nafasi ya Fasihi katika Kusawiri Suala la Dini”. *Kiswahili.* 79(1): 66-77.

Mosha, E.S. (2022) “Matumizi ya Sitiari katika Kazi za Fasihi: Mifano kutoka Nyimbo za Kivunjo”. *Kioo cha Lugha,* Juz. 20(1):18-35. DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i1.2

Mulokozi, M.M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu.* Dar es Salaam: KAUTTU.

Ngunyi, S.K. (2017) *Uchunguzi wa Vipengele Teule vya Fani katika Mashetani wa Alepo*. Tasinifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadhari na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njoroge, M.G.S. (2001) *Dhamira za Kidini katika Fasihi ya Kiswahili.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

O'Donoghue, D. (1957) "Book Review: Le Mal et L'Existence". *Irish Theological Quarterly*, Juz. 24: 368 - 369. https://doi.org/10.1177/002114005702400417.

Odhiambo, A.R. na Mutiso K. (2021) "Urudiaji wa Kisarufi Katika Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari Bin Darimi". *East African Journal of Swahili Studies*, Juz. 3(1): 100-107. https://doi.org/10.37284/eajss.3.1.404

Pamplany, J., Kaviyil, P., Olikkarottu, T. na Mari, J. (Wah) (2021) *Introduction to Theology*. Alpha Institute, Theology and Science. Kannur, Kerala.

Pohle, J. (2009) *Grace, Actual and Habitual* (Toleo la 3). Toronto: W. E. Blake & Son, Limited

Sartre, J.P. (2007) *Existentialism Is a Humanism*. Yale University Press.

Sartre, J.P. (2008) *Being and Nothingness*. London: Routledge.

Scheeben, M.J. (2024) *Nature & Grace*. Ohio: Emmaus Road Publishing.

Senkoro, F.E.M.K. (2011) *Fasihi Andishi*. Dar es Salaam: Kauttu Ltd.

Tariq, M. (2018) "Style, stylistics and stylistic analysis: A re-evaluation of the modern-day rhetorics of literary discourse. *International Journal of English Research,* Juz. 4(2): 46-50.

Trilling, L. (2008) *The Liberal Imagination: Essays on Literature and Society*. New York: Viking Press.

Wamitila, K.W. (2004) *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Publications Ltd

Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

Wamitila, K.W. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.

Watson, J.L.S. (2022) The Study of Religion and Theology in the Twenty-First Century: Boundaries and Encounters. Cambridge: Cambridge University Press.

Wood, W. (2021) *Analytic Theology and The Academic Study of Religion*. Oxford: Oxford University Press.

Wyschogrod, E. (1982) "God and "Being's Move" in the Philosophy of Emmanuel Levinas". *The Journal of Religion*, Juz. 62(2):145 - 155. https://doi.org/10.1086/486931.